

Haki Zako za Makao na Ruzuku ya Kodi ya Nyumba Jijini Iowa

Kuanzia tarehe 1 Juni 2016, wenye nyumba na mawakala wa nyumba Jijini Iowa hawawezi kukubagua eti kwa sababu upo katika mpango wa Vocha za Ruzuku za Nyumba (Sehemu ya 8). Kijitabu hiki kinakupa muhtasari wa haki zako za kupata makao.

Mei 2016



(Vocha za Ruzuku za
Nyumba/Sehemu ya 8)

NINASHIRIKI KATIKA MPANGO WA VOCHA ZA RUZUKU ZA NYUMBA (HVC). (MAARUFU KWA JINA 'SEHEMU YA 8') JE, HAKI ZANGU NI ZIPI?

Sheria za Haki ya Makao jijini lowa zinakulinda dhidi ya ubaguzi unaoweza kufanywa na wenye nyumba, madalali pamoja na wengine wanaohusika katika ukodishaji. Unalindwa ikiwa umekuwa katika mpango wa HCV kuanzia tarehe 1 Juni 2016.

Sheria za haki ya makao inaharamisha ubaguzi wa kutopata nyumba kwa misingi ya umri, rangi, mtazamo, ulemavu, utambulisho wa jinsia, hali ya ndoa, hali ya familia, nchi ya asili, kabila, dini, jinsia, mwelekeo wa ngono, kuwa au kutokuwa na wanaokutegemea au kupata msaada wa kifedha kutoka kwa serikali.

JE, NINAWEZA KULINDA HAKI ZANGU VIPI?

- Angalia nyumba kisha uamue kama ungependa kuikodisha kabla ya kutuma ombi.
- Beba jedwali la kuonyesha kima cha juu cha kodi (MGR) unapoenda kutafuta nyumba. Sehemu ya "TTP" iliyo kwenye fomu inaonyesha uwezo wako wa kodi na unaweza kuitumia kuhesabu uwiano wa mapato na kodi.
- Usiingie katika nyumba kama haijakaguliwa na kuidhinishwa na Mamlaka ya Makao.

JE, ULINZI WA HCV UNAPATIKANA KWA AJILI YA NYUMBA ZOTE ZA KUKODISHA KATIKA KAUNTI YA JOHNSON?

Hapana. Nyumba zilizo katika vitongoji vya jiji la lowa pekee ndizo zinahusishwa. Nyumba nyingine zilizo katika Kaunti ya Johnson hazina sifa za kupata ulinzi wa HCV. Wenye nyumba na wasimamizi katika maeneo mengine ya Kaunti ya Johnson wanaweza kukataa vocha.

JE, NITAJUAJE KAMA MTU ANANIBAGUA?

- Anapotangaza kwamba 'Sehemu ya 8 Haziruhusiwi.'
- Anapokataa ombi lako kwa sababu unatumia vocha au ruzuku nyingine ya kulipia kodi.

JE, NI LAZIMA MWENYE NYUMBA ANIPANGISHIE KWA SABABU NINA VOCHA?

Hapana. Ni sharti utume ombi na uonyeshe kwamba unaweza kulipa mgawo wako wa kodi, kuwa jirani mwema na kulinda nyumba. Lakini mwenye nyumba hawezi akaongeza matakwa ya ziada kwa lengo la kuwafungia nje wanaotumia HCV.

MWENYE NYUMBA AU MSIMAMIZI ANAWEZA AKAKUKATAA KIHALALI KWA SABABU:

- Una historia mbaya ya kulipa madeni.
- Historia ya jinsi ulivyofukuzwa kwingine.
- Maoni mabaya kutoka kwa wanaokujua.

Ukiwa mpangaji, unatakiwa kufuata mkataba na matakwa mengine ya mpango, kulipa kodi kwa wakati na kudumisha nyumba katika hali nzuri.

Mwenye nyumba au msimamizi anatarajiwa kukupa huduma kulingana na mkataba na kuhakikisha nyumba ni nzuri, salama na safi.

NIFANYE NINI IKIWA NIMBAGULIWA KATIKA KUPATA MAKAO?

Wasiliana na mamlaka ya Haki za Binadamu Jijini lowa moja kwa moja. Ikiwa unataka kuwasilisha malalamiko, ni sharti uripoti kabla ya kuisha kwa siku 300 tangu lilipotokea. Hata hivyo, tunakuhimiza uwasilishe ripoti haraka uwezavyo. Andika kilichotokea, lini kilifanyika, waliohusika, lini tukio lilitokea, walioshuhudia na maelezo mengine unayoweza kukumbuka. Hifadhi nyaraka zozote zinazohusiana na tukio. Kwa maelezo zaidi kuhusu haki zako za makao, wasiliana na mamlaka ya Haki za Binadamu la Jiji la lowa kupitia humanrights@iowa-city.org, 319-356-5022 au 319-356-5015. Unaweza kupata maelezo zaidi kwenye www.icgov.org/humanrights.